MASUALA YA UKUAJI:
SHERIA NA MAADILI

SIKU YA PILI
Mradi wa ushirikiano wa ustawi wa jamii kuhusu UKIMWI kwa ajili ya watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi.

Maisha Ya Mtoto 1

Makuzi Ya Binadamu Na Kujenga Ukaribu

Malengo

Mwisho wa siku, msaidizi ustawi wa jamii atakua na uwezo wa:

- Kueleza mahitaji ya watoto, wakiwemo wale waishio katika mazingira hatarishi
- Kueleza maeneo matano ya ukuaji wa mtoto
- Kueleza umuhimu wa ukaribu katika makuzi ya mtoto na mchakato wa kujenga ukaribu na mtoto
- Kueleza miongozo ya maadili kwa wasaidizi ofisa ustawi wa jamii

Malengo

- Elezea haki mahususi za mtoto kwa mujibu wa sheria za kimataifa na za ndani
- Elezea vipengele muhimu vya Mpango wa Gharama Nafuu wa Kuhudumia Watoto Yatima na Waishio Katika Mazingira Hatarishi
- Elezea sera na sheria za msingi zinazohusu watoto waishio katika mazingira hatarishi ikiwemo Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009

Ni yapi mahitaji ya msingi kwa Mtoto?

Bungua Bongo

Mahitaji Ya Msingi.....

- Malezi
- Chakula na lishe
- Hifadhi na Malazi
- Ulinzi dhidi ya unyanyasaji
- Msaada wa kisheria
- Huduma za kiafya
- Msaada wa kisaikolojia
- Msaada wa kielimu
- Mahitaji ya kiuchumi

Ukuaji Wa Binadamu

- Ukuaji wa binadamu hutokea katika maeneo matano (5):
  - Kimwili: Kuongezeka na kubadilika.
  - Kiakili: Uwezo wa kujifunza na kutatua matatizo.
  - Kihisia: Uwezo wa kutofautisha na kudhibiti mihemko.
  - Kijamii: Uwezo wa kujenga na kuendeleza uhusiano na watu wengine.
  - Kimaadili: Uwezo wa kujenga tabia kutokana na mfumo wa kuamini ili kujua lililo sahihi na lisilo sahihi.

Ukuaji Wa Binadamu .....

Hatua za ukuaji wa mtoto

- Kuzaliwa
- Uchanga
- Kutambaa
- Kabla ya kuanza shule
- Umri wa kuanza shule
- Kabla ya kubalehe
- Umri wa Kubalehe
- Kijana

Ukuaji Wa Binadamu

- Ukuaji wa binadamu huchangiwa na mazingira na vinasaba (genes).
- Kila mtoto hurithi vinasaba kutoka kwa wazazi wake, ambavyo vinamfanya kuwa wa pekee, tofauti na binadamu wengine lakini wote ni sawa.
- Watoto huhitaji malezi na matunzo kwa miaka mingi.

Ukuaji Wa Binadamu

- Kuna tofauti kubwa za kiukuaji kwa binadamu, kila mmoja wetu anakua katika kasi tofauti.
- Ukuaji huenda hatua kwa hatua . Na kila hatua ni muhimu kwa ajili ya inayofuata. Hakuna hatua inayoweza kurukwa.
- Huathiriwa na Kabila na tamaduni husika, elimu, muonekano na uzoefu katika maisha.

Ukuaji Wa Binadamu

- Ingawa kuwepo kwa tofauti kubwa kiukuaji kwa binadamu ni kawaida, kudumaa au kuchelewa kukua kunaweza kuashilia uwepo wa tatizo.
- Mshituko wa maono (trauma) na hata msongo wa mawazo (stress) huweza kuchelewesha maendeleo ya ukuaji na hata kurudisha nyuma ukuaji.
- Kuchelewa kufika hatua fulani ya ukuaji haimaanishi mtoto hatafikia hatua nyingine ya ukuaji. Ili kufikia hatua hiyo mzazi au mlezi (mwangalizi) anahitaji kuwa mvumilivu na mwangalifu.

Kiini Cha Nadharia Ya Kujenga Ukaribu (Attachment Theory)

Ili mtoto aweze kuja kuwa mtu mzima mwenye tabia nzuri na afya, anahitaji kukua katika mazingira ya mahusiano endelevu na mtu mzima anayejali na kusikiliza, ambaye mtoto anamuona kuwa ni mzazi wake.

Umuhimu Wa Kujenga Ukaribu

- Makuzi mazuri yanategemea sana mazingira aliyolelewa mtoto.
- Watoto wanahitaji kulelewa kwa upendo na kujaliwa ili kuwa na uwezo wa kujenga mahusiano salama, kujali na ya kudumu watakapokuwa watu wazima.
- Watoto walio wengi wamezaliwa katika familia zenye angalau mtu mzima mmoja au wawili ambao hujenga mapenzi (hisia) sahihi na za kudumu kwa mtoto.

Vipengele Muhimu Vya Ukaribu

- Mahusiano ya karibu ya muda mrefu na mtu fulani
- Uhusiano huu huleta hali ya usalama, amani na furaha
- Kupoteza au kuwa na hatari ya kupoteza mtu mmoja katika mahusiano huleta hali ya mfadhahiko
- Uhusiano wa aina hii mara nyingi huwa kati ya mzazi na mtoto

Umuhimu Wa Kujenga Ukaribu

- Ukaribu, upendo, na kujitoa kwa wanafamilia hujenga mazingira ya makuzi mazuri
  - Mtoto ambaye amejenga ukaribu na wazazi ana msingi mzuri wa kujenga uaminifu katika mazingira yake na kwa wale wanaomzunguka
  - ***Mtoto ambaye amejenga ukaribu na wazazi ana msingi mzuri wa kujifunza, kujenga upendo na makuzi mazuri kijamii***

Jinsi Ya Kujenga Ukaribu

- Mazoea ya ukaribu: kushikwa, kuimba, kulisha, kutazama machoni, kubusu na tabia nyingine zenye kuashiria ukaribu
- Vigezo muhimu katika kujenga uhusiano thabiti hujumuisha kukaa pamoja/kuwa na muda wa kuwa pamoja (utotoni), kuongea ana kwa ana, kumtazama mtoto usoni mnapoongea, kuwa karibu/kukaribiana, kugusa, na njia zingine zinazogusa hisia kama vile harufu, sauti, na muonjo.

Jinsi Ya Kujenga Ukaribu

- Wanasayansi huamini kuwa kigezo muhimu katika kujenga ukaribu ni pamoja na mgusano chanya (mfano kukumbatia, kubeba na kucheza)
- Kubeba watoto, kuwatazama, kutabasamu, kubusu, kuimba na kucheka husisimua kemikali katika ubongo ambazo zinahusika katika kuufanya ubongo kujenga ukaribu kati ya mtoto na mlezi.

Masuala Yahusuyo Ukaribu

- Ijapokuwa ukaribu ni muhimu katika miaka ya uchanga, ukaribu na mzazi ni muhimu katika kipindi chote cha utoto
- Kukosa au kutojenga ukaribu wakutosha husababisha matatizo katika maisha yote ya mtu

Hatua Za Ukuaji Wa Mtoto

Umri wa kwenda Shule
Kabla ya Kubalehe
Umri wa Kubalehe

Zoezi

- Tutaona tofauti gani katika maeneo yafuatayo kwa namna ambavyo mtoto atakabiliana na hali ngumu kulingana na umri wake?
  - Kimwili
  - Kijamii
  - Kihisia

Fanyeni hili zoezi katika kundi kubwa au dogo

Zoezi

- Watoto wa umri wa kwenda shule (miaka 6-10)
- Kabla ya umri wa kubalehe (miaka 10-12)
- Umri wa kubalehe (miaka 13-17)
- Ujana (miaka 18-24)

Fanya hili zoezi katika kundi dogo au kubwa

Watoto Wa Umri Wa Kwenda Shule

- Watoto wa umri wa kwenda shule-ishara kuu:ukuaji kimwili mara nyingi hutokea polepole
  - Kuongezeka kwa uwezo wa kufanya kazi za mikono pamoja na kuongezeka kwa uwezo wa kuzungumza, akili na maadili
  - Wasichana na wavulana hawatofautiana katika njia ya kukua
  - Uwezo wa kufanya shughuli mbalimbali huongezeka kadri umri unavyoongezeka

Watoto Wa Umri Kabla Ya Kubalehe

- ***Watoto wa umri kabla ya kubalehe-*** Ishara Kuu: mwanzo wa homoni kubadilika
  - Kiwango cha kukua huongezeka
  - Ukuaji usiolingana unaweza kuathiri tabia
  - Majukumu kati ya wasichana na wavulana huanza kutofautiana
  - Tabia huathiriwa na kubadilika kwa homoni
  - Kutaka kuwa tofauti na kutotegemea wazazi huongezeka

Umri Wa Kubalehe

- ***Umri wa kubalehe-*** Ishara kuu: Kuongezeka kwa kasi ya kukua kwa homoni na kimaumbile
  - Kasi ya ukuaji uendelea kupungua. Kwa wasichana hufika kikomo kwenye miaka 16 na wavulana miaka 18-20
  - Ukuaji kimaumbile hukamilika na majukumu kati ya wasichana na wavulana hutofautiana
    - Majukumu ya kikazi huendana na maumbile (me au ke) lakini pia kufuatana na mila na desturi
    - Kuendelea kujitofautisha na kupunguza kuwategemea wazazi huendelea kwa kiwango kikubwa katika umri huu
  - Makuzi ya kiakili na kimaadili huanza kukaribia ya mtu mzima

Ujana

- ***Ujana***
  - Makuzi ya kimwili na kiakili kwa vijana hufikiwa katika umri wa miak 25
  - Ukuaji wa akili unakua umekamilika na kuruhusu watu wazima kuweza kujipangia muda, kukua kiimani na kukabiliana na mambo mengi katika maisha

Rejea

- Pastor., Blome, W., Cavin, B., Langan, J., Leighton, M., McFadden, E., Olea, M. Petras, D., Polowy, M., Ryan, P.,Sweency-Springwater, J., & Wynne, S. (1993).
- *FosterPRIDE/AdoptPRIDE: Preparation and assessment program for foster and adoptive families*. Washington, DC: CWLA. The Costed MVC Action Plan, 2007 - 2010. The Government of Tanzania. 2008 (FHI)

HAKI ZA WATOTO

Masuala ya Kimaadili na kisheria

1. Masuala ya Kimaadili na kisheria

- Ni nini maana ya maadili?
- Sheria ni nini?
- Ni nini maana ya haki za binadamu?

Bungua bongo

Tofauti Kati Ya Maadili Na Haki

- ***Maadili***:Taratibu/Miongozo
- ***Haki***: Sheria au kanuni

Maadili Ya Msaidizi Afisa Ustawi Wa Jamii

- Jali utu na hadhi ya kila mmoja.
  - Wasaidizi wa afisa ustawi wa jamii wanatakiwa kutambua na kuheshimu utu wa kila mmoja/familia kama alivyo kwani hakuna mtu anayefanana na mwingine
  - Wasaidizi afisa ustawi wa jamii wanatakiwa kutetea na kuheshimu kila mtoto na utu wake
- Tambua umuhimu wa mahusiano na binadamu wengine
  - Wasadizi afisa ustawi wa jamii wanatakiwa kutambua ya kwamba binadamu hawaishi na kufanya kazi wenyewe/peke yao

Maadili Ya Msaidizi Afisa Ustawi Wa Jamii

- Onyesha kuwa mwaminifu
  - Msaidizi Afisa Ustawi wa Jamii anatakiwa kuwa mfano, atende haki, mkweli na muwazi katika kazi zake na watoto pamoja na familia
- Heshimu haki ya kila mtu kujiamulia
  - Mara zote kwa kadiri iwezekanavyo, msaidizi afisa ustawi wa jamii aheshimu haki za watoto waishio katika mazingira hatarishi kuweza kufanya maamuzi yao binafsi ili mradi tu hayaingilii haki za wengine.

Maadili Ya Msaidizi Afisa Ustawi Wa Jamii

- Kuchochea haki za watoto walio katika mazingira hatarishi kushiriki katika maamuzi yanayowahusu
  - Watoa huduma wahimize ushiriki kamilifu wa watoto waishio katika mazingira hatarishi na kutoa huduma kwa njia ambayo itawajengea uwezo wa kujiamulia katika nyanja mbalimbali za maisha yao
- Kumchukulia kila mtoto kama mtu aliyekamilika
- Tunatakiwa kuhusika na mtu kama alivyokamilika ndani ya familia, jamii, na mazingira yake na tuhakikishe tunaelewa kila nyanja ya maisha ya mtoto

Maadili Ya Msaidizi Afisa Ustawi Wa Jamii

- Pambana na upotoshaji wa haki katika jamii
  - Wasaidizi afisa ustawi wa jamii wasimame imara katika kutetea haki za watoto waishio katika mazingira hatarishi ikiwa ni pamoja na kupambana na aina zote za unyanyapaa na kutengwa.
- Chochea haki za kiuchumi
  - Wasaidizi afisa ustawi wa jamii watambue tofauti za kiuchumi zilizopo kati ya wanaume na wanawake, hususani katika ngazi ya kaya/familia k.m mgawanyo na utumiaji mali usio sawa.

Maadili Ya Msaidizi Afisa Ustawi Wa Jamii

- Heshimu siri na mipaka yake
  - Ustawi wa Jamii wana jukumu la kuweka siri/faragha taarifa za wateja wao isipokuwa kwa ridhaa ya mterja mwenyewe au pale ambapo inaaminika ya kwamba kutotoa siri kutamnyima haki mteja au watu wengine
- Tufanye kazi kulingana na taaluma zetu na uwezo wetu
  - Wasaidizi wa afisa ustawi wa jamii wana jukumu la kufanya kazi katika mipaka ya taaluma na stadi zao na kulingana na mradi au programu. Kwa mfano, usifanye ushauri nasaha kwani hiyo sio taaluma yako
- Huduma kwa wengine iwe kipaumbele
  - Wasaidizi wa afisa ustawi wa jamii wanapaswa kuweka maslahi ya watoto/familia anazohudumia mbele ya maslahi binafsi

2. Haki Ya Kijamii

- Watoa huduma wana wajibu wa kuinua haki katika jamii, kulingana na jamii kwa ujumla na WYWMH wanaowahudumia.

Haki Ya Kijamii

***Hii ina maana**: -*

Kupinga ubaguzi

- Ni wajibu wetu kupinga ubaguzi kwa WYWMH kwa vigezo vya uwezo, umri, utamaduni, jinsia na jinsi.
- Ni muhimu kutambua na kuheshimu tofauti za makabila na tamaduni mbalimbali katika jamii, kwa kuangalia watu binafsi, familia, makundi na jumuia mbalimbali.

Haki Ya Kijamii

- Lazima tuhakikishe kuwa rasilimali zilizopo kwa ajili yao zinagawiwa kwa usawa, kulingana na mahitaji.
- Program zote za watoto lazima zihamasishe haki na matakwa yao na kulinda utu wao.
- Maslahi ya mtoto lazima yapewe kipaumbele cha kwanza.
- Haki za mtoto kufanya uamuzi kwa masuala yake lazima iheshimiwe siku zote.

Haki Ya Kijamii

- Umakini lazima ufanyike ili kuhakikisha kwamba watoto wanaelewa maana ya wao kushiriki.
- Watoto lazima wawezeshwe ili waelewe kwamba wanaweza kuamua kushiriki au la.
- Hakuna mjadala, ni lazima kuhakikisha kwamba watoto wana haki ya kuweka siri mambo yao na hawatengwi.
- Watoto ni lazima washiriki wakiwa katika mazingira ambayo wanajisikia salama na marika yao, na ambapo hawatajisikia kutishwa, kuogopeshwa au kutumikishwa.

Haki Ya Kijamii

- Watoto hawatakiwi kutazamwa kwa muonekano hasi au kuonyeshwa kwamba wanahali mbaya.
- Watoto hawatakiwi kunyonywa kwa sababu za kibiashara, tiba au tafiti.
- Watoto, wazazi na walezi lazima washirikishwe katika kutengeneza sera ili sera hizo ziwe zinamlenga mtoto.

Haki Za Mtoto

- “Kwa kuzingatia kwamba mtoto anatakiwa aandaliwe kikamilifu kuishi maisha yake yeye binafsi katika jamii na kulelewa katika hali muafaka kama inavyoainishwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa, hususani katika misingi ya amani, heshima, uvumilivu, usawa na mshikamano”.

Utangulizi: Mkataba wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki za Mtoto.

Mkataba Wa Haki Na Ustawi Wa Mtoto Wa Afrika

Mkataba wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa Afrika ni andiko linalotoa haki fulani na upendeleo kwa watoto wa Afrika.

Haki Za Kisheria Za Watoto

- Kuna mikataba ya kimataifa mingi inayozungumzia haki za watoto. Mhimu zaidi katika hii ni Mkataba wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki za Mtoto.
- Sheria zinazohusu haki za mtoto katika nchi mbalimbali zinatofautiana sana kama ilivyoainishwa katika katiba za nchi hizi.
- Watu wanatakiwa kuijua sheria na inatakiwa kutekelezwa**.**

Mkataba Wa Umoja Wa Mataifa Wa Haki Za Mtoto

Mkataba huu una kanuni kuu nne:

- Haki ya mtoto kuhusu maisha, kuishi, na maendeleo.
- Haki ya mtoto ya kutendewa kiusawa. Hii ina maana mtoto ***asibaguliwe.***
- Haki ya mtoto ***kushiriki*** katika shughuli na maamuzi yanayowahusu.
- Vitendo vyote lazima vizingatie ”masilahi ya mtoto”.

Mkataba Wa Umoja Wa Mataifa Unajumuisha

- Haki ya jina.
- Ulinzi kwa mtoto asiye na familia.
- Haki ya Utaifa.
- Ulinzi katika kazi ambazo zinamadhara katika afya, elimu na maendeleo ya mtoto.

Mkataba Wa Umoja Wa Mataifa Unajumuisha

- Ulinzi dhidi ya unyanyasaji na kukataliwa/kutengwa.
- Ulinzi dhidi ya kunyonywa kingono.
- Haki ya huduma za afya na matibabu.
- Uhuru wa mawazo, kujua baya na zuri, na Dini.

Haki Za Kikatiba Za Mtoto Wa Kitanzania

i) Maisha, kuishi, na maendeleo (Kif. 3).
ii) Kuheshimiwa (Kif. 12)
iii) Kujiunga na jumuia na kushiriki katika mikusanyiko ya amani.
iv) Kupata elimu ya msingi na sekondari.
v) Kujieleza kama mtu binafsi.

Haki Za Kikatiba Za Mtoto Wa Kitanzania.

vi. Uhuru wa mawazo kujua jema na baya, na dini (Kif. 14)
vii Uhuru wa kujumuika na mikusanyiko ya amani (Kif. 15)
viii Watoto wana haki ya kujiunga katika jumuia na makundi mengine kama vile umoja wa vijana,vyama vya kisiasa, skauti, na makundi mengine.
ix. Ulinzi wa faragha (Kif. 16)
x. Kupata habari zinazowahusu (Kif.17)
xi. Haki ya kutopata mateso au ukatili, kuteswa au adhabu isiyo ya kawaida (Kif. 37 (a)

Haki Za Kikatiba Za Mtoto Wa Kitanzania.

- Watoto wanahitaji ulinzi maalumu kwani hawana uwezo wa kujilinda wenyewe dhidi ya mateso na unyanyasaji.
- Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998 imeongeza kifungu katika kanuni ya adhabu, kifungu 169A kuhusu ukatili kwa watoto, kulinda watoto kuhusu kunyanyaswa, kubaguliwa na kuumizwa.

Sheria Muhimu Zinazowalenga Watoto Yatima Na Waishio Katika Mazingira Hatarishi Tanzania

- Sheria ya Hakia za Mtoto Na.21 2009
  - Sheria hii inabadilisha sheria nyingine zilizohusu mtoto na kuzijumuisha katika sheria moja. Inalinda haki na kuchochea ustawi wa mtoto kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa na ya kikanda; inatoa mwongozo juu ya uasilishaji, malezi ya kambo na ulinzi wa mtoto.

Wajibu Wa Mtoto Wa Tanzania

Kwa mijibu wa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 mtoto wa Tanzania ana wajibu wa:

- Kuhifadhi umoja wa familia
- Kuheshimu wazazi, walezi, na wakubwa zake wakati wote, pamoja kuwasaidia wakati wa mahitaji
- Kutumikia jamii yake na taifa kwa ujumla kwa nguvu na uwezo kiakili kufuatana na umri wake.
- Kulinda na kuimarisha umoja wa kijamii na kitaifa; na
- Kulinda na kuimarisha mila na desturi njema katika jamii yake na taifa kwa ujumla

Sheria Muhimu Zinazowalenga Watoto Yatima Na Waishio Katika Mazingira Hatarishi Tanzania

- Sheria ya Makosa ya Kujamiiana 1998(SOSPA)
  - The Law prohibits any forced sexual relationship, example any sexual relationship with a person under 18 years old is considered as a forced sexual relationship/raped. Sheria hii inakataza mahusiano ya kimapenzi ya kulazimisha, k.m. muhisiano yoyote ya kimapenzi na mtu aliye chini ya umri wa miaka 18 yanatafsiriwa kuwa ya kulazimisha
- Sheria ya Kuzuia Maambukizi ya VVU/UKIMWI 2009.
- Sheria ya elimu na Ufundi Stadi.

Sheria Muhimu Zinazowalenga Watoto Yatima Na Waishio Katika Mazingira Hatarishi Tanzania

- Sheria ya Kupinga Usafirishaji Haramu wa Binadamu 2008.
  - Sheria hii inakataza usafirishaji haramu wa binadamu pamoja na watoto. K.m, kumsafirisha mtoto kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa misingi ambayo ni kinyume na haki za mtoto kama vile, kwenda kufanya kazi haramu, ukahaba, uchuuzi, kufanya kazi baharini, machimboni, ubebaji wa mizigo, kufanya kazi katika viwanda vinavyotengeneza/kutumia sumu kali, kufanya kazi katika sehemu za starehe kama vile baa, na hoteli
- Sheria ya Uendeshajhi Mashtaka
  - Sheria inatafsiri aina ya adhabu kwa makosa mbalimbali ya jinai

Sera

- Sera ya Mtoto na Maendeleo 2008.
- Mwongozo wa Kitaifa kwa Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi, 2006
- Sera ya Elimu
- Sera ya Afya
- Sera ya Maendeleo ya Vijana 2007
- Sera ya Ulemavu 2003
- Sera ya Kuzuia Maambukizi ya VVU/UKIMWI 2001

Pitio La Mpango Wa Taifa Wa Utekelezaji Wenye Gharama Nafuu Kuhusu Matunzo, Msaada Na Ulinzi Wa Mtoto 2007-2010.

Utangulizi

Programu za Tanzania zimetokana na:

- Kikao Maalumu cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kiliazimia;Ifikapo 2005 kila nchio iwe na mikakati ya kusaidia programu za UKIMWI na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ikilenga maeneo yafuatayo
  - Mpango wa utekelezaji wenye gharama nafuu wa kuhudumia watoto waishio katika mazingira hatarishi
  - Mfumo wa uratibu na usimamizi wa mipango inayohusu watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi
  - Mfumo wa Sera wa kisheria
  - Mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji na tathimini (Mfumo wa kumbukumbu na takwimu)
  - Mfumo shirikishi wa kitaifa wa tathimini na ufuatiliaji
  - Tamko na shirika la kazi duniani dhidi ya utumikishaji wa watoto

Utangulizi

- Mkataba wa Kimataifa wa haki za mtoto1989
  - Inatoa mwongozo wa haki na ustawi wa mtoto.
- Malengo ya Maendeleo ya milenia
  - Lengo namba 1,2, 3, 4, &6- Kupunguza umasikini, elimu ya msingi, umoja, kupunguza vifo vya watoto, kuzuia maambukizi ya VVU/UKIMWI na magonjwa mengine ya kuambukiza

Usuli

- Mkataba wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa Afrika-1990.
  - Mkataba huu unaendana na ule wa umoja wa mataifa lakini unaongeza haki na majukumu ya mtoto wa Afrika
- Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA).

Nia Ya Mpango Wa Gharama Nafuu

- Kutoa mwelekeo na mwongozo katika juhudi na shughuli mbalimbali zinazolenga kuwalinda, kuwahudumia watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi nchini.
- Kutambua wadau na kupanua wigo wa utekelezaji wa shughuli za yatima na watoto walio katika mazingira hatarishi na maeneo makuu yaliyoainishwa kwa kuangalia nani ,wapi na kwa kiasi gani.

Nia Ya Mpango Wa Gharama Nafuu

- Utafutaji, uratibu na upatikanaji wa rasilimali ndani na nje.
- Kutoa na kuweka wazi mambo ya kufanywa na wadau mbalimbali kwa kushauri kutumia mbinu ,mikakati ili kujua nani,wapi,lini,wanufaikaji na gharama.

Vipengele 8 Katika Mpango

- Sera na mazingira ya utoaji huduma
- Huduma na msaada katika ngazi ya kaya
- Elimu
- Huduma ya Afya ya Msingi
- Ulinzi na usalama
- Mahitaji ya kisaikolojia
- Kujengea uwezo jamii na utafutaji rasilimali.
- Ufuatiliaji na tathmini

Sera Na Mazingira Ya Huduma

- Kushawishi serikali kuunga mkono
- Kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma (Kitaifa, Mkoa, Wilaya na Kijiji)

Sera Na Mazingira Ya Huduma

- Majukumu ya Idara ya Ustawi wa Jamii, Wizara nyingine na taasisi mbalimbali zinazohusika na masuala ya watoto.
- Sera na mipango.
- Utetezi na uhamasishaji jamii.

Huduma Na Matunzo Katika Ngazi Ya Kaya

- Uhakika na hifadhi ya chakula na lishe
- Makazi (kuwepo kwake na ubora wake)
- Malazi na mavazi
- Usafi wa mtu binafsi
- Malezi na makuzi ya mtoto.
- Malezi ya kambo na kuasili, na kuwepo kwa watoa huduma.

Elimu

- Programu za elimu ya awali (vituo vya kulelea watoto wadogo mchana(day care centers), elimu ya awali (pre primary school)
- Elimu ya msingi na sekondari
- Elimu ya ufundi stadi

Huduma Ya Afya.

- Ukuaji na maendeleo ya mtoto(IMCI)kudhibiti magonjwa ya watoto kwa uwiano, na kuzuia maambukizi ya VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto
- Huduma za afya (matunzo na matibabu), huduma ya matibabu majumbani kwa watoto wanaoishi na VVU/UKIMWI.
- Upatikanaji wa maji safi na salama
- Usafi wa mazingira.

Mahitaji Ya Kisaikolojia

- Ni vitu gani ambavyo mtoto aliye katika mazingira hatarishi anahitaji ili aijisikie kuwa anajaliwa kihisia na kijamii

Bungua bongo

Mambo Yanayosaidia Kufanya Mtoto Ajihisi Kuwa Anajaliwa

- Upendo na kupendwa
- Kutambuliwa
- Usalama
- Kuthaminiwa
- Kukubalika
- Kusifiwa
- Kushirikishwa
- kuaminiwa

Ulinzi Na Usalama

- Vyanzo vya usalama na ulinzi(Safety nets)
- Ushiriki wa watoto
- Hifadhi ya jamii
- Haki za mtoto katika jamii
- Stadi za maisha

Kupima Matokeo Ya Mpango Wa Kitaifa (Ufuatiliaji Na Tathmini)

- Kuwepo na mfumo wa ufuatiliaji na tahmini.
- Kujengea uwezo jamii.
- Rasilimali (kuwepo na mfumo wa upatikanaji na utumiaji wa rasilimali)

Washirika

- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.
- Wizara na idara zinazohusika na masuala ya watoto
- Mashirika ya kiraia
- Wadau wa maendeleo na mashirika ya umoja wa mataifa mf.UNICEF, USAID, DFID,WB

Uratibu

- Kamati elekezi ya kitaifa ya watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi.
- Kamati ya kiufundi ya kitaifa ya watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi.
- Kikundi cha wadau watekelezaji (implementing partners group)

Kazi Za Kujenga Stadi

- Ili kuwa Msaidizi Afisa ustawi wa jamii unapaswa kujifunza stadi kwa njia ya vitendo
  - ***Msaidizi afisa ustawi wa jamii hujifunza kupitia:***
    - Majadiliano
      - Kubungua bongo
      - Majadaliano katika makundi makubwa
      - Visa mkasa
      - Maigizo
      - Mbinu nyingine za kukazia maarifa na kujenga stadi

Kitabu Cha Kujifunzia Stadi

- Fungua kitabu chako cha kujifunzia stadi
- Utakua unafanya kazi za kupeleka nyumbani kila siku katika kitabu hiki
- Kila siku unapofika kwenye mafunzo unapaswa kumpatia mmoja wa wakufunzi kitabu chako wakati wa mapunziko ya chai
- Mkufunzi atapitia kazi yako atatoa alama na kukupa mrejesho.
- Unatakiwa kumaliza kazi 4 kati ya 5 ili uweze kufuzu mafunzo haya

Kazi Za Makundi

- Hesabu moja mpaka nne. Kila namba ni kundi moja. Hesabu hadi kila mtu awe na kundi. Kila kundi litapewa kisa cha kupitia (Rehema, Koku, Tumaini, au Amani)
- Mtakijadili hicho kisa kila siku kwenye kikundi
- Mtapata fursa ya kukazia mlichojifunza kwenye darasa kwa njia ya kazi ya kikundi
- Kikundi kitajadili masuala ya msingi kwa ujumla kwa dakika kumi na tano. Andika mada muhimu kutokana na hayo majadiliano na pia kwa kutumia kitabu chako.
- Baada ya majadiliano mtafanya kazi ya kikundi ambayo inaweza kujumuisha kujigawa katika makundi madogo zaidi ili kufanya igizo au mbinu nyingine ya kukazia maarifa

Kazi Za Makundi

- Jadili mlichojifunza kutokana na kazi ya kikundi na mada ya siku
- Jaribu kuandika kwa kifupi mlichojifunza mkawasilishe kwenye darasa siku inayofuata
- Mrejesho usiwe zaidi ya dakika tano na usiwe na zaidi ya MAMBO MATANO MUHIMU
- Usirudie kuelezea kila kitu kuhusu visa vilivyojadiliwa

Mrejesho Wa Kazi Za Makundi

- Mrejesho uandikwe na wanakikundi kuzingatia waliyokubaliana
- Mrejesho uzingatie stadi mlizojifunza kutokana na mada za siku iliyopita. Msitoe maelezo mengi sana juu ya kisa mlichojadili

Kazi Za Vikundi

Siku Ya 2: Kazi Za Vikundi: Kutambua Watoto Na Familia Zilizo Katika Mazingira Hatarishi

- Pitia kisa cha kikundi chenu na mjaribu kujifunza stadi za utambuzi na kuwafikia watoto waishio katika mazingira hatarishi
- Fanya igizo la utambuzi katika kijiji
  - Igizo linaweza kuwa na: Msaidizi afisa ustawi wa jamii, viongozi wa kijiji, wanafamilia, polisi, majirani, watoa huduma za afya na watoto
- Katika mchakato wa utambuzi, jiulize kama utaanza kuwafikia kwanza viongozi wa kijiji(serikali ya kijiji, viongozi wa kimila, viongozi wa kidini, nk) ili ikusaidie katika utambuzi
- Tumia fomu ya utambuzi kupanga mchakato mzima wa utambuzi na kuwafikia familia
- Chagueni mtu mmoja ambaye atawasilisha kazi ya kikundi kwenye darasa kesho saa mbili na nusu asubuhi. Mrejesho uelezee mchakato wa kuwafikia na kuwatambua watoto waishio katika mazingira hatarishi